

The  
Management  
University  
of Africa



Sponsored by the Kenya Institute of Management

**UNDERGRADUATE UNIVERSITY EXAMINATIONS**  
**SCHOOL OF MANAGEMENT AND LEADERSHIP**  
**DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION ARTS**

**ECT 227: SPECIAL SUBJECT METHODS AND MICRO TEACHING:  
KISWAHILI**

**TAREHE: 1<sup>ST</sup> APRILI 2026**

**MUDA: MASAA MAWILI**

**JUMLA YA ALAMA: 70**

**MAAGIZO:**

1. Andika nambari yako ya usajili katika kitabu cha majibu ulichopewa.
2. **USIANDIKE CHOCHOTE** kwenye karatasi ya maswali
3. Karatasi hii ya mtihani ina maswali **sita (6)**
4. **SWALI LA KWANZA** ni la lazima
5. Jibu maswali mengine **MATATU** kutoka sehemu zilizobaki.
6. **SWALI LA KWANZA** lina alama **25** ilhali maswali mengine yana **ALAMA 15** kila moja.
7. Jibu majibu yako yote katika kitabu cha majibu/ mtihani ulichopewa.

### SWALI LA KWANZA

a) Jadili umuhimu wa kuandaa rekodi ya kazi unapofunza lugha  
( alama 10)

b) Fafanua stadi nne kuu zinazofundishwa katika mtaala wa elimu  
nchini Kenya.

(alama 4)

c) Wewe ni mwalimu wa lugha wa kidato cha tatu na unafunza somo  
la sarufi kuhusu aina za maneno. Andika mpangilio wa somo  
(andao la somo) litakalochukua dakika 40.

(alama 11)

### SWALI LA PILI

a) Kwa kurejelea Misingi ya Nadharia ya Mawasiliano, onyesha ni kwa  
namna gani nadharia hii humwezesah mwalimu kufunza lugha ya pili.

(alama 8)

b) Eleza umuhimu wa kutayarisha maazimio ya kazi katika kufunzia  
Kiswahili.

(alama

7)

### SWALI LA TATU

a) Mpangilio wa somo ni nini?

(alama

3)

b) Jadili vipengele au vijenzi mbali mbali vinavyopatikana katika  
mpangilio wa kipindi kwa mwalimu wa lugha ya Kiswahili.

alama 12)

### SWALI LA NNE

a) "Silabasi ya Kiswahili ina umuhimu wa kipekee kwa mwalimu wa  
Kiswahili." Eleza.

(alama

5)

- b) Ni matatizo yepi ambayo yanaweza kumkumba mwanafunzi anayesoma ufahamu kwa sauti. **(alama 5)**
- c) Eleza ni kwa namna ipi wewe kama mwalimu wa lugha ya Kiswahili utaweza kutatua matatizo ambayo yanaweza kuwakumba wanafunzi wanaosoma kwa sauti. **(alama 5)**

### SWALI LA TANO

Kwa kutolea mifano mwafaka, onyesha umuhimu na udhaifu wa mbinu zifuatazo za kufundishia stadi mbali mbali katika lugha ya Kiswahili.

a) Majadiliano

**(alama 8)**

b) Kufunza katika makundi.

**(alama 7)**

### SWALI LA SITA

a) Jadili malengo/ya kufunza lugha ya Kiswahili nchini Kenya.

**(alama 6)**

b) Pambanua aina tatu za uainishaji wa malengo /shahaba ya funzo unapoandaa mpangilio/andao la somo.

**(alama**

**9)**